# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 047 NOVEMBA 2024

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 WADAU WA BAHARI WAKUMBUSHWA MATUMIZI SAHIHI YA HUDUMA ZA HALI YA HEWA

## 2 DKT. CHANG'A AELEZA MCHANGO WA PROGRAMU ZA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC) KWA NCHI ZINAZOENDELEA



## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI DISEMBA, 2024



## KITAIFA

# WADAU WA BAHARI WAKUMBUSHWA MATUMIZI SAHIHI YA HUDUMA ZA HALI YA HEWA

**Dar es Salaam**




Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) iliwakumbusha wadau wa bahari na maziwa makuu matumizi sahihi ya huduma za hali ya hewa kupitia Kongamano na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jumuiya ya Mamlaka za Usimamizi na Usafirishaji kwenye Maji Barani Afrika uliofanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere ( JNICC) - Dar es Salaam kuanzia tarehe 29 Novemba hadi 01 Disemba 2024.

TMA imekuwa na mchango mkubwa kwa wadau wa Sekta ya Bahari na katika Maziwa Makuu katika kusaidia kuokoa maisha ya watu na mali kwa ujumla hususan katika kipindi hiki ambapo Dunia inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, ikiambatana na matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo joto kali, upepo mkali, vimbunga, mvua kubwa na mafuriko. Changamoto ambazo zimekuwa na athari za moja kwa moja kwa watumiaji wa Bahari na maziwa makuu.

Wadau mbalimbali walipata fursa ya kuuliza maswali na kutoa michango yao kwa lengo la kuboresha huduma zao na hivyo kuongeza tija kwa maendeleo endelevu ya Taifa na Dunia kwa ujumla.





KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A AELEZA MCHANGO WA PROGRAMU ZA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC) KWA NCHI ZINAZOENDELEA

**Baku, Azebaijan**




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, alieleza mchango wa programu za Jopo la IPCC ambazo ni pamoja na Programu ya IPCC ya Ufadhili wa Masomo (IPCC Scholarship Programme) katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi hususan katika nchi zinazoendelea zikiwemo nchi za bara la Afrika.

Dkt. Chang'a aliyasema hayo tarehe 18 Novemba, 2024 alipochangia kwenye mdahalo kuhusu "Uimarishaji wa elimu ya kukabiliana na Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (Enhancing Climate Change Education, Awareness and Climate Action), ulioandaliwa sambamba na Mkutano Mkuu wa 29 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "United Nations Framework for Convention on Climate Change Conference of Parties (UNFCCC COP29) ", uliofanyika Jijini Baku, Azerbaijan tarehe 11 hadi 22 Novemba, 2024.

Akichangia katika mdahalo huo, Dkt. Chang'a alisema programu za Jopo la IPCC, hususan Mfuko

wa IPCC (IPCC Trust Fund) na Programu ya Mafunzo ya IPCC (IPCC Scholarship programme) zimekuwa na mchango mkubwa katika kujenga uwezo wa wataalamu na hivyo kusaidia jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na Tabianchi hususan katika nchi zinazoendelea, zikiwemo nchi za Bara la Afrika. Alitoa mfano wa Programu ya Mafunzo ya IPCC kuwa imeendelea kusaidia kutoa ufadhili wa masomo ya elimu ya juu, na hivyo kuchangia katika kuimarisha uwezo wa vijana wengi katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

"Programu ya Mafunzo ya IPCC imetoa mchango wa pekee katika kujenga na kuimarisha uwezo wa wanasayansi wanaochipukia, hususan katika bara la Afrika". Alisema Dkt. Chang'a na kutoa wito kwa Wadau wote wakiwemo Washirika wa Maendeleo kuchangia fedha katika programu ya IPCC Scholarshp pamoja na Mfuko wa IPCC Trust Fund. Aidha, Dkt. Chang'a alieleza mchango wa Taarifa mbalimbali za Tathmini ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi zinazoandaliwa na Jopo hilo la IPCC katika maamuzi tangu taarifa hizo zianze kutolewa mwaka 1990.

Sambamba na mdahalo huo, Dkt. Chang'a alishiriki pia katika vikao na semina mbalimbali za kutoa elimu kwa vijana na wanasayansi wanaochipukia, ambapo aliwahamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, pamoja na kazi za Tathmini ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi zinazofanywa na Jopo hilo, hususan Tathmini ya Saba ambayo mchakato wake ulianza mwaka jana 2023.

Katika hatua nyingine, Dkt. Chang'a alifanya kikao na Katibu Mkuu wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Prof. Celeste Saulo ambapo walijadili kuhusiana na uboreshaji wa huduma za hali ya hewa katika bara la Afrika kwa kuwezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa zaidi ya akili mnemba (Machine Learning and Artificial Intelligence) katika kuboresha zaidi utabiri wa hali ya hewa na huduma za tahadhari.

Ushiriki wa Dkt. Ladislaus Chang'a katika shughuli za IPCC zilizoandaliwa sambamba na mkutano wa COP29 ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya Makamu Mwenyekiti wa Jopo la IPCC.



TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI DISEMBA, 2024

Mvua zinatarajiwa kendelea katika maeneo mengi nchini katika kipindi cha Disemba, 2024. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini kutokana na kuimarika kwa Ukanda mvua. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuendelea kujitokeza hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Vipindi vya mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Vipindi vya mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza ya mwezi.** |

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO SEKTA YA HALI YA HEWA

## Mfumo wa uangazi wa hali ya hewa wa anga la juu

Mamlaka imefunga mfumo mpya wa uangazi wa hali ya hewa ya anga ya juu katika kituo cha kupima hali ya hewa ya anga ya juu kilichopo JNIA ili kuimarisha upatikanaji wa data za hali ya hewa ambazo ni muhimu kwa ajili ya usalama na ufanisi wa usafiri wa anga.









## JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Mathew Ndaki

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.